



## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJI KISARAWE



Agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuupatia mji wa Kisarawe maji kutoka katika Mtambo wa Ruvu Juu linatekelezwa kazi kwa kasi.

Kazi inayoendelea hivi sasa ni uchambuzi wa zabuni zilizowasilishwa na kufunguliwa mwishoni mwa wiki iliyopita ambapo jumla ya kampuni 12 za ndani na nje ya nchi zilijitokeza.

Kazi zilizofanyika kabla ya zabuni kutangazwa ni pamoja na kukamilishwa kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi, kuandaa makabrasha ya zabuni na kutangaza zabuni hizo.

Awamu ya kwanza ya mradi huu mkubwa itahusisha kazi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa kituo cha kusukuma maji kitakachokuwa na uwezo wa kufungwa pampu nne, ununuzi na ufungaji wa pampu mbili zenye uwezo wa kusukuma maji kiasi cha lita 60 kwa sekunde kwa kima cha mita 180 na kujengwa kwa kituo cha kupokea maji chenye uwezo wa kuhifadhi lita 480,000. Mji wa Kisarawe upo katika muinuko na ili maji yaweze kufika kutoka katika tenki la Kibamba kituo cha kusukuma maji kitahitajika kujengwa.

Mradi pia utahusisha ununuzi na ulazaji wa mabomba makuu ya kipenyo cha milimita 400 kwa umbali wa kilometa 17 kwenda katika makao makuu ya Wilaya na bomba lenye kipenyo cha milimita 300 kwa umbali wa kilometa 3.5 kutoka katika bomba kuu kwenda katika eneo lililotengwa kwa ajili ya viwanda. Aidha mtandao wa mabomba ya ugawaji maji ya kipenyo cha milimita 200 kwa urefu wa kilometa 15 yatalazwa katika maeneo mbalimbali ili kuboresha usambazaji maji kwa watumiaji wa maji Mjini Kisarawe.

Ili kuhakikisha kuwa maji yanagawanywa kwa uwiano mzuri matenki mawili yatajengwa katika awamu mbili tofauti. Tenki la kwanza lenye ujazo wa lita milioni nne litajengwa eneo la Mnarani kwa ajili ya matumizi ya makazi yaliyopo na

awamu ya pili itahusisha ujenzi wa tenki la Vigungu ambalo litahudumia eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi mapya na nyongeza ya maji kwa ajili ya viwanda vitakavyoongezeka.

Matarajio ni kumpata Mkandarasi mwanzoni mwa mwezi wa tatu ili kazi za ujenzi zianze ndani ya mwaka huu wa Fedha.

Hata hivyo katika hatua ya muda mfupi ya kupunguza tatizo la maji katika mji huo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia DAWASA inatekeleza mradi wa maji wa Vigama ambapo kisima kipya kimechimbwa. Mkandarasi wa kufunga pampu, kujenga mnara, kufunga tenki la kuhifadhi maji na kulaza mabomba la kusambaza maji hayo amepatikana na ujenzi utanza mwezi Februari 2018 na kumalizika Aprili 2018. Aidha DAWASA inatarajia kukarabati kisima cha Shule ya Sekondari Maneromango ikiwa ni mchango wake katika mkakati wa kuboresha miundombinu ya shule ili kuongeza ufaulu katika Wilaya hiyo. Utaratibu wa kumpata mkandarasi wa kazi hii upo katika hatua za mwisho na matarajio ni kuanza kazi hii Machi 2018.

**IMETOLEWA NA OFISI YA UHUSIANO NA JAMII DAWASA**